JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI**

# DHANA YA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI




**MACHI, 2017**

**YALIYOMO**


1. DHANA YA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI (COM)
2. UMUHIMU WA KUSHIRIKISHA JAMII
3. MISINGI MIKUU YA DHANA YA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI YAKE
4. KANUNI ZA KUPATIWA HUDUMA YA MAJI KUFUATIA UHITAJI WA JAMII (DRA)
5. MANTIKI YA DHANA YA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI YAKE YENYEWE NA SUALA ZIMA LA SERA
6. LENGO NA MKAKATI WA COM NA DRA
7. JINSI YA KUJENGA DHANA IMARA KWA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI YAO
8. VIASHIRIA VYA JAMII KUWA NA UHITAJI WA MRADI
9. HITIMISHO

## *1.* DHANA YA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI (*Community Ownership and Management COM)*

### Lengo la somo:

Washiriki kuelewa umuhimu wa dhana ya jamii kumiliki, kuendesha na kusimamia miradi yao. Hii itasaidia washiriki kuelewa ni kwanini dhana hii inatumika na pia kuongeza ujuzi sahihi wa namna gani jamii inaweza kushirikishwa katika hatua zote za utekelezaji na usimamizi wa miradi katika ngazi ya kijiji.

Msingi mkuu wa jamii kuonyesha uhitaji na kupatiwa miradi (***DRA***) katika sekta ya maji vijijini ni swala zima la jinsi gani jamii inamiliki na kusimamia huduma ya maji katika eneo husika. Dhana ya jamii kumiliki miradi inamaanisha jamii inapaswa inufaike kutokana na huduma ya maji kwakutekeleza majukumu yao, kuwa na mamlaka ya mradi, kudhibiti maendeleo ya mradi wao na kuweza kuufanyia matengenezo.

Dhana ya jamii kumiliki miradi yao itawezekana tu pale ambapo jamii itashirikishwa katika hatua zote za utekelezaji, ushirikishwaji huu sio jambo la mara moja au siku moja, linapaswa kuwa endelevu mpaka pale jamii itakapoweza kusimamia huduma ya maji na kuwa endelevu.

## 2. KWANINI NI MUHIMU KUSHIRIKISHA JAMII

- Uzoefu unaonyesha kuwa ushirikishwaji jamii katika hatua zote za utekelezaji wa mradi husababisha jamii kufanya maamuzi sahihi, jamii kuchangia gharama za mradi kwakutoa nguvu kazi zao au kwa fedha taslimu ambapo hupelekea jamii kuutumia kuuendeleza mradi wao.

Jinsi gani jamii itaweza kushiriki

- Kwa kushiriki moja kwa moja katika mikutano, kutoa maoni, na katika shughuli mbalimbali zinazohitaji jamii kujitolea
- Kwa kuwa ni vigumu kwa jamii yote kushiki katika mambo yote basi ni vema jamii kuchagua watu watakaowawakilisha katika kutekeleza majukumu ya mradi, mfano kuwa na Kamati yenye uwakilishi mzuri na yenye uwezo wa kuwakilisha mawazo ya jamii husika.

i. Hapo awali jukumu la kupanga, kujenga na kusimamia miradi ya maji vijijini lilikuwa jukumu la Serikali Kuu na Washirika wa

Maendeleo, bila ushirikishwaji wa wana jamii husika. Mfumo huu haukuonyesha mafanikio makubwa ndipo Serikali ikaona ni vema kuanzisha dhana ya umiliki wa miradi kwa wana jamii wenyewe

ii. Vivyo hivyo ilionekana kuwa ushirikishaji wa jamii katika Programu ya Maji haukuwa mzuri na mipango mingi ilifanywa na Waratibu kutoka nje ya jamii husika. Hii ilipelekea kutokufanikiwa kwa malengo ya mipango ya maji vijijini

iii. Matokeo yake miradi mingi haikumilikiwa na jamii wala kufanyiwa matengenezo kwa wakati na kusababisha miradi mingi kuharibika na kusimama kutoa huduma ya maji

iv. Dhana ya jamii kumiliki na kusimamia miradi ya maji vijijini inamaanisha kuwa, jamii husika itakaa pamoja na kufanya maamuzi ya ni nini wanahitaji, kipi kinahitajika ili kuweza kukidhi hitaji lao, ni kwa kiasi gani wanaweza kumudu na hatimae kufanya maamuzi sahihi katika maswala ya teknolojia sahihi kwao kwakulinganisha uwezo wao katika kumudu uendeshaji na matengenezo.




Jamii ikipanga na kujadili namna sahihi ya kusimamia miradi yao.

## 3. MISINGI MIKUU YA DHANA YA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI YAKE (*Community Ownership and Management Principles; COM*)

i. Jamii imiliki miradi yao na kuwajibika katika swala zima la uendeshaji, matengenezo na kuitunza
ii. Jamii kufanya maamuzi ya jinsi gani wanataka kusimamia miradi yao
iii. Jamii kuipa nguvu kamati/chombo kinachosimamia miradi yao katika kufanya maamuzi na kuchukua hatua hitajika kwa niaba yao
iv. Wanawake wanakuwa na uwakilishi sahihi katika Kamati/Chombo Simamizi na kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi.
v. Kamati ina uwezo wa kusimamia na kurekebisha pale panapotokea matatizo, wahudumu wa mradi wanapewa mafunzo katika jamii ili kuwa na uwezo wa kufanya matengenezo madogomadogo na kwa

matengenezo makubwa jamii inakua na uwezo wa kumwita fundi mwenye uwezo atakayelipwa na jamii yenyewe.

vi. Jamii inakusanya fedha kwa ajili ya kununulia vipuri, mafutaya kuendeshea mitambo na kulipia matengenezo.

vii. Jamii inasafisha na kusimamia maeneo ya mradi.

viii. Jamii ina fanya kazi kwa pamoja na inatumia mradi wao kwa maji safi ili kuboresha afya zao.

ix. Jamii inachukua hatua katika kuhakikisha ina endeleza afya na usafi wa mazingira katika nyumba zao na eneo la mradi.

## 4. KANUNI YA JAMII KUPATIWA HUDUMA YA MAJI VIJIJINI KUFUATIA UHITAJI WALIONAO (*Demand rResponsive Approach; DRA*).

Kuna kanuni kuu tano katika utekelezaji wa huduma ya maji vijijini

i) Maombi kutoka kwa jamii

Jamii lazima iwe na uhitaji wa huduma, sambamba na hilo jamii lazima iwe na taarifa muhimu ni kwa namna gani wanaweza kushiriki na kutimiza wajibu wao katika kuhakikisha waendeleza mradi wao. Mradi unatakiwa uweke taratibu na kuzitekeleza ili kuhakikisha taarifa za kutosha zinawafikia jamii na kwakutumia njia sahihi. Kufutia zoezi hili jamii itatuma maombi ya mradi wa maji kwa kuainisha nia na uwezo walio kufuatia dhana ya jamii kupatiwa miradi kulingana na uhitaji walio nao na kutekeleza wajibu na majukumu yao.

### ii) Uwezo wa jamii

Mara nyingi jamii huwa ina mapungufu katika uwezo wa kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Timu ya mradi inapaswa iainishe uwezo na mapungufu uliopo ndani ya jamii ili kuweza kujenga uwezo na kuboresha pale ambapo panaonekana pana upungufu kabla ya kuanza kutekeleza mradi. Vyombo vya Watumia Maji ni lazima Viundwe na kusajiliwa na pia kujengewa uwezo katika ngazi zote za utekelezaji wa mradi.

### iii) Aina za teknolojia

Jamii lazima ishirikishwe katika uchaguzi wa teknolojia ya mradi itakayotumika. Jamii lazima ieleweshwe aina mbalimbali za teknolojia zilizopo na kiwango cha huduma (service level) kitakachotolewa kwakuzingatia gharama za uendeshaji na matengenezo.

### iv) Uchangiaji gharama

Taratibu za uchangiaji wa gharama za miradi ya maji ni lazima zifafanuliwe vizuri mapema kwa wadau wote. Utayari wa jamii katika kuchangia gharama za miradi ya maji ni kiashiria muhimu kinachoonyesha uhitaji kutoka kwa jamii na utayari huo ndio utakaoifanya jamii iwe na umiliki mzuri wa mradi wao. ushirikishwaji jamii katika kuchangia gharama za miradi hasa wakati wa ujenzi kwakutoa nguvu kazi zao au kwakutoa fedha kwa kiwango walichokubaliana. Uchangiaji lazima uelezwe kwa namna ambayo jamii itaweza na watakuwa na utayari nao.

### v) Umiliki mradi na jukumu uendeshaji na matengenezo

Swala na umiliki wa mradi, kuchangia gharama za uendeshaji na matengenezo, kupanga na kukubaliana bei ya maji, gharama za kununua mradi mpya baada ya mradi kuchakaa na kuisha muda wake ni lazima ziainishwe na zipangiliwe vizuri wakati wa kubuni mradi husika.

## 5. MANTIKI YA DHANA YA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI YAKE YENYEWE NA SUALA ZIMA LA SERA

**i.** Miradi ya maji na usafi usafi wa mazingira wanayopewa jamii bila ya wao kushirikishwa kikamilifu katika hatua zote za utekelezaji wa mradi, siyo endelevu. Umiliki wa miradi ikiwa ni pamoja na visima vya maji kama haitamilikishwa kwa jamii kisheria bado miradi hiyo haitadumu. Sababu hizi hupelekea jamii kukosa dhamira ya kusimamia na kuendesha miradi yao, dhana ya jamii kumiliki na kusimamia miradi yao wenyewe huwezesha jamii kuanzisha, kumiliki na kusimamia miradi yao.

**ii.** Toka kuanzishwa kwa Sera ya Usambazaji Maji ya mwaka 1991 Mabadiliko mengi yalijitokeza katika Sekta ya Maji, yakitilia mkazo zaidi katika swala zima la ushiriki mkamilifu wa jamii, Sekta Binafsi na Serikali za Mitaa / Halmashauri kuwa na jukumu kubwa la kutoa huduma na kuondoa jukumu hilo kwa Serikali Kuu. Mapungufu makubwa ya sera ya usambazaji maji ya 1991 Serikali Kuu ilikuwa na jukumu lote la utekelezaji na usimamizi wa miradi.

**iii.** Kwa sababu hizo ulazima wa kupitia kwa upya Sera ya Maji ya Mwaka 1991 ulionekana ambapo Muundo wa Kifanisi wa Kisheria na kiuitekelezaji wake uliainishwa. Sera ya maji ya Mwaka 2002 ilizinduliwa, ambayo inalenga kuhakikisha jamii na mnufaikaji

anashirikishwa katika hatua zote za mipango, ujenzi, uenedeshaji na matengenezo ya miradi ya maji.

Sera ya Maji ya Mwaka 2002, jamii ni wamiliki, wapangaji, watekelezaji, Wasimamizi na watumiaji wa miradi iliyokamilika, hii ndiyo tunaweza kusema DHANA YA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI YA MAJI.

## 6. LENGO NA MKAKATI WA COM NA DRA

### i) COM (Dhana ya jamii kumiliki na kusimamia miradi yake)

- Dhana ya jamii kumiliki na kusimamia miradi yake ni kiini cha Mkakati wa RWSSP. Jamii iko katikati ya mchakato, wanachagua, wanapanga, na kujenga miradi yao, pale wanapojenga watamiliki na kuwajibika katika kuusimamia na kuendeleza.

### ii) DRA (Mbinu shirikishi za kupanga na kuamua vipaombele vya Jamii)

- Kwa asili, jamii kuainisha mahitaji yao ina maana kuwa, utoaji wa huduma unalenga katika kufanya maamuzi yenye uelewa ambayo yanalenga katika nini watumiaji wanahitaji, uwezo wa kulipia (kulingana na gharama ya mradi) na wanakuwa na uwezo wa kutunza na kuendeleza kwa watumiaji kuuchangia kwa fedha taslimu au kwa kulipia kwa ulichonacho ambayo itakidhi garama za uendeshaji na matengenezo.

## 7.JINSI YA KUJENGA DHANA IMARA KWA JAMII KUMILIKI NA KUSIMAMIA MIRADI YAO

Unaweza kujenga dhana imara kwa jamii kumiliki na kusimamia miradi yao kama yafuatayo yatazingatiwa

i. kuhakikisha mradi wa maji unamilikiwa kisheria na jamii husika.
ii. Kukubaliana na muundo husika wa taasisi ambayo itaonyesha kila mdau katika sehemu yake ana wajibu na kazi gani
iii. Kuandaa mwongozo wa jinsi gani kila mtu atafanya wajibu wake kwa kushirikiana na wenzake kama Kamati Tendaji,jamii ya Watumiaji Maji, Halmashauri, Wakandarasi binafsi na waajiriwa wa mradi katika suala la Kisera na mikakati yote
iv. Kuandaa taratibu na sheria zitakazoelekeza ni kwa jinsi gani kila Mdau atatekeleza wajibu wake

v. Kuhakikisah wajumbe wote wanafikia mwafaka katika mfumo wa uwazi na uwajibikaji ikiwepo taarifa na tathmini ya maendeleo ya mradi na

## 8. VIASHIRIA VYA JAMII KUWA NA UHITAJI WA MRADI

i. Jamii lazima ipeleke maombi kuonyesha uhitaji wa mradi husika
ii. Ada ya utayari ilipwe na pia akaunti ya benki ifunguliwe kuonyesha utayari wa kiuchumi kushiriki katika mradi husika.
iii. Kamati iundwe ili kuihamasisha jamii kushiriki vema katika mradi husika
iv. Mkataba wa Uendeshaji (MOU) usainiwe na wanajamii na waleta mradi.
v. Viongozi wa Serikali mfano Mwenyekiti wa Mtaa, Diwani na/Afisa Mtendaji wa Kata waonyeshe utayari wao kushiriki kwa hali na mali kuhakikisha mradi unatekelezeka.